

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITHANI
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

630

MBINU ZA KUFUNDISHA SAYANSI

Muda: Saa 3

Alhamisi, 13 Mei 2010 Mchana

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C.
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na B na maswali mawili (2) kutoka sehemu C.
3. Sehemu A ina alama 36, sehemu B ina alama 40 na sehemu C ina alama 24.
4. Simu za mkononi haziruhusiwi katika chumba cha mtihani.
5. Andika Namba yako ya Mtihani katika kila ukurasa wa kitabu chako cha kujibia.

SEHEMU A (Alama 36)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. (a) Fasili mtajo andalio la somo.
(b) Nini umuhimu wa andalio la somo kwa mwalimu wa somo la Sayansi?
2. Walimu wawili wanajadiliana. Mwalimu mmoja anasema ni vizuri kufundisha Sayansi kwa njia ya vitendo au majaribio. Mwalimu mwingine anasema, hujui kuwa watoto wa shule za msingi wana umri mdogo mno? Wewe kama mwalimu toa sababu nne (4) zinazomuunga mkono mwalimu wa kwanza.
3. Nini faida na hasara ya kutumia mbinu ya ziara-mafunzo katika kufundisha somo la Sayansi?
4. Eleza tofauti mbili (2) kati ya muhtasari na azimio la kazi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Sayansi.
5. (a) Nini maana ya zana za kufundishia?
(b) Orodhesha sifa nne (4) za zana nzuri ya kufundishia.
6. (a) Kwa nini walimu hawatumii majaribio ya kisayansi kama njia ya kufundishia? Toa sababu mbili.
(b) Eleza mambo mawili muhimu ambayo mwalimu wa Sayansi anatakiwa kuzingatia anapotathmini wanafunzi wanaofanya jaribio la kisayansi.
7. Taja vifaa vinne (4) vya mtaala wa somo la Sayansi.
8. (a) Watu wengi wanapobeba mizigo kichwani hutumia kata. Kata huwekwa katikati ya mzigo na kichwa. Kama mwalimu wa Sayansi eleza ni kwa nini wanafanya hivyo.
(b) Orodhesha madhara matatu yanayoweza kutokea wakati wa ufundishaji na ujifunzaji endapo zana hazikuandaliwa vizuri.
9. “Si vizuri kutaja jina la mwanafunzi kabla ya kuuliza swali”. Toa sababu mbili (2) za kuunga mkono hoja hiyo.

SEHEMU B (Alama 40)

Jibu maswali **mawil (2)** kutoka sehemu hii.

10. (a) Andaa andalio la somo unaloweza kutumia unapofundisha mada ya chakula bora kwa wanafunzi wa darasa la tano.
- (b) Ni kwa nini watu wanadhani kuwa somo la Sayansi ni gumu kufundisha? Toa sababu tano (5) kutetea hoja ya kuwa somo la Sayansi ni gumu katika ujifunzaji wake.
11. (a) Eleza hatua ambazo mwalimu anayetaka kutumia njia ya ziara-mafunzo anatakiwa kuzingatia.
- (b) Mwanafunzi mmoja alienda ufukweni mwa bahari. Alipofika alidondosha shilingi na ikazama. Mwanafunzi alishangaa kuona meli kubwa na yenye mizigo mingi ikipita kwenye maji bila kuzama. Wewe kama mwalimu wa sayansi toa maelezo kwa huyu mwanafunzi yanayoweza kumuondolea utata utokanao na hali hiyo.

SEHEMU C (Alama 24)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

12. Eleza jinsi utakavyoandaa jaribio kwa wanafunzi wa darasa la sita kuhusu kusafiri kwa joto kwa njia ya mpitisho. Jadili utakavyoandaa vifaa vya kufundishia mada hiyo.
13. Jadili mambo sita (6) muhimu ya kuzingatiwa wakati wa kutathmini mada ya Sayansi iliyokwisha fundishwa.
14. Jadili faida na hasara za kutumia kazi mradi, katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Sayansi.
15. Kwa kutumia sifa za mbegu, eleza njia tatu za kutawanya mbegu zenye sifa ulizotaja.